**SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)**

**(SURA YA 287)**
**SHERIA NDOGO**

(Zimetungwa chini ya kifungu cha 88 sura na. 287)

**SHERIA NDOGO YA UANZISHAJI WA MFUKO WA AFYA YA JAMII (CHF) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA KAKONKO, 2015**

**Jina** 1. Sheria ndogo hii itajulikana kama Sheria ndogo za (Uanzishaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii) Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko mwaka 2015 na zitaanza kutumika mara baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

**Matumizi** 2. Sheria ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya Halmashauri ya Wilaya.

**Tafsiri** 3. Katya Sheria ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo:
**"Ada ya mtumiaji"** maana yake ni ada anayolipa mtumiaji wa huduma kwa hospitali, Kituo cha Afya au Zahanati, kwa ajili ya huduma ya Afya iliyotolewa kwa mtumiaji:

**"Asasi"** maana yake ni pamoja na shule,Vyuo, vikundi mbalimbali vilivyosajiliwa kwa mujibu wa sharia au asasi yoyote itakayokuwa imekubaliwa na Kuidhinishwa na Bodi.

**Sura ya 287**

**"Bodi**" maana yake ni ni chombo kinachosimamia Huduma za Afya ya Halmashauri iliyoundwa kwa mujibu wa kifungu Na.58 cha sharia ya serikali za mitaa(Mamlaka za wilaya) sura Na.287

**"Halmashauri"** maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko.

"**Huduma za Afya"** mmana yake ni huduma zote za Afya zinazotolewa na Hospitali za serikali na watu binafsi na zinajumuisha huduma nyingine za Afya zilizoanzishwa kwa madhumuni ya kutoa huduma za Afya ikiw ni pamoja na vituo vya Afya na zahanati;

**"Kadi"** maana yake ni kadi itakayolewa kwa mwanachama wa mfuko wa Afya ya Jamii (CHF);

**"Kaya"** maana yake ni Baba, Mama na watoto walio chini ya umri wa miaka kumi na minane(18),mtu yeyote aliyetimiza miaka kumi na nane na Zaidi au Asasi;

**"Kituo cha Huduma kilichoteuriwa"** maana yake ni kituo kinachotoa Huduma za Afya kinachomilikiwa na Halmashauri,Serikali,asasi ya kidini,mtu au watu binafisi ambacho kinahusika na mfuko wa Afya ya jamii;

"**Mchango"** maana yake ni mchango wa fedha wa hiari,utakaotolewa na wanachama wa mfuko mfuko wa Afya ya jamii (CHF);
Mganga Mkuu wa Wiraya"maana yake ni daktari ambaye ni musimamizi Mkuu wa shughuli zote za huduma za afya katika Halmashauri ya Wilaya;

"**Mwanachama"**maana yake ni kaya iliyochangia huduma za mfuko wa Afya ya jamii(CHF);

"**Malipo ya Huduma**" maana yake ni malipo yanayolipwa katika kituo cha kutolea Huduma za Afya kwa wasio wanachama wa Mfuko;

"**Wizara"**maana yake ni Wizara yenye dhamana ya masuala ya Afya;

**Mfuko wa Afya ya Jamii(CHF)**

4. (1) Kutakuwa na Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) ambao ni mfuko wa hiari wenye lengo la kutoa huduma za Afya, ambapo mwanachama atakuwa akilipia huduma hizo kabla ya kuugua na Serikali itatoa mchango wake wa fedha kama jazilizo kwa mchango kutoka kwa mwanachama; **(Tele kwa tele).**

(2) Matumizi ya fedha yatafanywa na kusimamiwa na Bodi kwa mujibu wa sharia ndogo hizi

**Madhumuni ya Mfuko** 5. Madhumuni ya mfuko huu yatakuwa ni:-

(a) Kutafuta vyanzo vya fedha kutoka katika jamii kwa ajili ya kutoa huduma bora za Afya kwa Mwanachama;
(b) Kutoa huduma bora za Afya zinazopatikana kwa kutumia mipango endelevu na
(c) Kuboresha huduma za Afya katka Jamii kwa kugawanya madaraka na kuzipa nguvu jamii katika kufanya maamuzi na kuchangia katika masuala yanayohusu Afya zao.

**Mratibu wa Mfuko wa Afya ya Jamii** 6. (1) Kutakuwa na Mratibu wa Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) wa Halmashauri atakayeteuliwa na Mkurugenzi Mtendaji Wilaya baada ya kupokea mapendekezo kutoka timu ya uendeshaji ya Halmashauri.

(2) Majukumu ya Mratibu wa Mfuko wa Afya ya Jamii yatakuwa kama ifuatavyo:-

a) Kufuatilia, kusimamia na kuratibu Uendeshaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) kwenye vituo vya kutolea huduma za Afya.
b) Kuwa kiungo kati ya Halmashauri, Jamii na Wadau mbalimbali kwa ushirikiano na mhasibu wa Mfuko, na
c) Kuandaa taarifa za Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) za robo na mwaka mzima pamoja na majukumu mengine atakayopangiwa na Halmashauri.

**Muundo wa Bodi** 7 (1).

Bodi itakuwa na Wajumbe wafuatao:-

a) Wawakilishi wane wa watumiaji huduma za Afya,kati yao wawilini lazima wawe ni wanawake;
b) Mwakilishi mmoja kutoka watoa huduma za Afya binafsi bila ya faida;
c) Mwakilishi mmoja kutoka watoa huduma za Afya binafsi kwa faida waliochaguliwa na Halmashauri ya Wilaya kutoka vituo vya kutolea huduma za Afya binafsi kwa faida waliochaguliwa miongoni mwao na
d) Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi,Afya na Huduma za Jamii

Wataalamu ambao hawatapiga kura:-

a) Afisa Mipango wa Halmashauri
b) Mganga Mkuu wa Halmashauri, ambae atakuwa katibu wa Bodi
c) Mwakilishi mmoja kutoka Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya endapo hakuna atatoka kwenye Hospitali Teule
d) Mwakilishi mmoja kutoka timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya ya Mkoa

Mwenyekiti wa Bodi atachaguliwa miongoni mwa Wajumbe waliotajwa kifungu (1) a-c hapo juu

**Sifa za Wajumbe wa Bodi** 8.

Mjumbe wa Bodi atakuwa na sifa zifuatazo;-

a) Awe raia wa Tanzania,sharti hili halitawahusu wajumbe kutoka mashirika yasiyo ya serikali.
b) Awe na umri wa miaka isiyopungua ishirini na moja na kuendelea
c) Awe amehitimu Elimu ya Sekondari na kuendelea
d) Awe na uzoefu na amewahi kuonyesha uwezo wake wa kuongoza katika shughuli za huduma ya jamii
e) Awe na hakili timamu
f) Asiwe amewahi kutiwa hatiani kwa koso lolote la jinai.
g) Asiwe na wadhifa wowote wa kisiasa kupitia chama chochote cha siasa,na
h) Awe mwanachama hai wa mfuko wa (CHF).

**Kazi za Bodi** 9 (1). Ili kufanikisha malengo yake makuu Bodi itakuwa na kazi zifuatazo:-

a) Itasimamia masuala na shughuli zote zinazohusu mfuko wa jamii (CHF)
b) Kusimamia Huduma za Afya katika Halmashauri,
c) Kushauriana na Timu ya Uendeshaji ya Huduma za Afya ya Halmashauri na kuhakikisha kuwa Huduma ya Afya ni Bora na ya kitaalamu,
d) Kukusanya na kusimamia mapato ya Mfuko wa Afya ya Jamii,
e) Kupendekeza kwa Halmashauri watu wanaostahili kusamehewa kutoa mchango kwenye mfuko,
f) Kuweka malengo ya Mfuko,
g) Kupitia ripoti na taarifa kutoka kamati ya Afya ya kata au Chanzo kingine chochote,
h) Kuratibu makusanyo,matumizi na kudhibiti mapato,na
i) Kupanga mipango ya Afya ya mwaka kwa ajili ya kuthibitishwa na Halmashauri;

**Muda wa kukaa madarakani**

10 (1) Mjumbe wa Bodi atakuwa Madarakani kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia tarehe ya uzinduzi wa Bodi na anaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi kingine cha miaka mitatu tu.

(2) Endapo nafasi yeyote ya Mjumbe wa Bodi itaachwa wazi kwa sababu ya kifo,kujiuzulu au kwa sababu nyingine yeyote ile,Mjumbe mwingine atachaguliwa kujaza nafasi hiyo iliyoachwa wazi.

(3) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha pili (2),haitaruhusiwa kuchagua mjumbe mwingine iwapo kipindi kilichobaki ni chini ya miezi sita.

**Akaunti ya Mfuko**

11 (1)Kutakuwepo na Akaunti maalumu itakayotumika na Halmashauri Ambayo fedha zote zitakazokusanywa kwa ajili ya mfuko zitahifadhiwa na kutolewa kulingana na miongozo iliyopo.

(2) Wawekaji saini wa Akaunti ya mfuko watachaguliwa na Bodi na Watakuwa ni:mmoja kutoka kundi "A" na "B" na kwa namna yeyote Ile hakuna pesa zitakazotolewa kwenye akaunti ya Mfuko bila saini Ya mmoja wapo kutoka kundi "A" na "B"

(3) Watia saini kwenye hundi za Mfuko watakuwa kama ifutavyo:-

(a)Mwenyekiti wa Bodi na Mjumbe mmoja wa Bodi ambao Watakuwa kundi "A"

(b)Katibu wa Bodi ambaye atakuwa ni Mganga mkuu wa Halmashauri na mweka Hazina wa Halmashauri ambao Watakuwa kundi "B"

(4) Kila baada ya miezi mitatu,Bodi itakuwa inaandaa na kutoa taarifa ya Akaunti ya mfuko na kuwasilisha kwa Halmashauri,

(5)Akaunti ya Mfuko wa itakaguliwa na Wakaguzi waliochaguliwa kwa mujibu wa Kanuni za Fedha za Serikali.

**Matumizi ya Fedha za Mfuko**

12 Fedha zitakazokusanywa na Mfuko zitatumika kwa Madhumuniyafuatavyo:-

(a) Masuala yanayohusiana na Afya yaliyotajwa katika mpango kabambe wa afya wa Halmashauri na kuidhinishwa na Halmashauri; na
(b) Suala au shughuli yeyote muhimu ya afya itakavyoonekana inafaa na kama itaidhinishwa na Bodi.
(c) Asilimia 30 ya mapato ya tele kwa tele ipelekwe kwenye akaunti ya kituo cha Rufaa cha Wilaya na Asilimia 70 itarudi kwenye vituo kwa ajili ya Matumizi.

**Vyanzo vya Mapato.**

13 Vyanzo vya mapato ya mfuko vitatokana na:-

(a) Fedha zote zitakazopelekwa kutokana na michango ya Wanachama
(b) Ruzuku kutoka kwenye Halmashauri,na Serikali kuu,
(c) Wahisani mbalimbali toka ndani na nje ya Halmashauri,
(d) Michango ya Watu binafisi wanaoishi ndani nan je ya Halmashauri,
(e) Malipo ya fedha ya wasiokuwa wanachama wa mfuko kwa kupata huduma ya afya,
(f) Ushuru utaotozwa na Halmashauri kutoka vyanzo mbalimbali na kutengwa kwa ajili ya Mfuko,
(g) Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya na
(h) Fedha zozote halali ambazo Mfuko unaweza kupata toka mahali pengine popote.

| | | |
|---|---|---|
| **Mipango** | 14 | (1) Bodi itaandaa mipango na bajeti ya mwaka kwa kuonyesha kiwango kinachotarajiwa kupatikana na mgawanyo wa Fedha kwa ajili ya utoaji huduma za afya na maendeleo katiaka maeneo ya Halmashauri kwa utaratibu unaotumika na Halmashauri.<br>(2) Bodi itapokea,itajadili,itachambua na kuidhinisha mpango wa afya na kuwasilishwa kwa Halmashauri kwa ajili ya kuidhinishwa kwa Halmashauri kwa ajili ya kuidhinishwa kwa kupitia Kamati za Halmashauri.<br>(3) Bodi itatoa maoni ya bajeti ya nyongeza kama kutakuwa na haja ya kufanya hivyo na kama mazingila yataruhusu;<br>(4) Mipango ya Bajeti ya mfuko itaandaliwa kulingana na utaratibu kama ilivyoainishwa katika vifungu vidogo vya (1) na (2) hapo juu,ambayo ni lazima iwasilishwe kwa Halmashauri kwa ajili ya kuidhinishwa. |
| **Usimamizi Wa Mfuko** . | (15) | Usimamizi na Uendeshaji wa Mfuko utakuwa chini ya<br>(a) Halmashauri ya wilaya,kupitia Bodi ya Huduma za Afya ya Halmashauri katika ngazi ya Halmashauri,<br>(b) Kamati ya Maendeleo ya kata kupitia Kamati ya Afya ya Kata,katika ngazi ya kata,na<br>(c) Halmashauri ya kijiji kupitia Kamati ya huduma za jamii ya Kijiji. |
| **Taarifa ya Fedha** | (16) | Bodi itatakiwa kuandaa taarifa ya mapato na matumizi ya fedha na kuwasilisha kwa Halmashauri kulingana na miongozo ya uandaaji wa Taarifa za fedha za Halmashauri. |
| **Kamati ya Afya ya Kata Sura ya 409** | (17) | Kutakuwa na Kamati ya afya ya Kata ; |

**Wajumbe wa Kamati ya Afya ya 409**

18. (1) Kamati ya Afya ya kata itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) Diwani anayewakilisha kata husika

(b) Afisa Mtendaji wa Kata

(c) Mwalimu Mkuu mmoja kutoka kwenye shule ya msingi ambayo ipo kwenye kata husika

(d) Wajumbe wawili watakaowakilisha jamii husika ambapo mmoja wao ni lazima awe mwanamke;

(e) Tabibu Mfawidhi au Tabibu Mfawidhi msaidizi ,wa kituo cha Afya au Zahanati,ambaye atakuwa Katibu wa Kamati,

(f) Mjumbe mmoja atakaye teuliwa na Kamati ya maendeleo ya kata kutokana na watu waliopendekezwa na kamati za kata aliyomo ndani ya eneo la kata ;na

(g) Mjumbe mmoja atayeteuliwa na kamati ya Maendeleo ya kata kutoka kwenye vyama vya kijamii kutoka kwenye kata.

(2)Mwenyekiti wa kamati ya Afya ya kata atachaguliwa kutoka miongoni mwa wajumbe.

(3)Endapo kamati ya afya ya kata itashindwa kutekeleza kazi zake,Bodi itatoa onyo au kuivunja na Halmashaurinitafanya utaratibu wa Uchaguzi wa wawajumbe wenginekatika muda usiozidi miezi mitatu.

**Kazi na majukumu Ya kamati ya Afya ya Kata**

. 19 (1)Kamati ya Afya ya kata itakuwa na majukumu yafuatayo;

(a) Kuhamasisha na kuandaa jamii kujiunga na mfuko wa Afya ya jamii (CHF),
(b) Kuandaa orodha na kuratibu idadi ya wanachama wa mfuko wa Afya wa jamii (CHF),
(c) Kusimamia ukusanyaji wa michango ya mfuko,
(d) Kuratibu viwango vya uchangiaji kwenye Huduma za Afya,
(e) Kupitia Utendaji wa Mfuko wa afya ya jamii na kutoa mapendekezo na ufumbuzi kwa Halmashauri kupitia Bodi ya Afya,
(f) Kuanzisha na kuratibu Mipango ya afya ya jamii na;
(g) Kuendesha mikutano ya wanachama wa mfuko wa Afya ya jamii (CHF) ndani ya kata.

(2)Kamati ya Afya ya kata,itakaa kila baada ya miezi mitatu (3)na katibu Atatoa taarifa ya maandishi siku saba (7) kabla ya siku ya kikao.

**Utoaji wa Huduma za Afya**

20. Kila mwanachama;

(a) Atakuwa na haki ya kisheria kupata huduma ya afya aliyolipia kabla ya kuugua ndani ya Halmashauri au eneo linguine lolote kwa kadri itakavyo kubaliwa,
(b) Atakuwa na haki ya kutoa mapendekezo kuhusu Huduma za Afya kupitia Kamati husika ambayo yatafanyiwa kazi na Bodi;na
(c)Atashirikishwa kikamilifu katika uandaaji na utekelezaji wa mpango wa upatikanaji wa Huduma za Afya katika eneo la Halmashauri.

| | | |
|---|---|---|
| **Kiwango cha Mchango au Ada ya Mwanachama** | (21) | (a)Mtu yeyote atakayetaka kuwa mwanachama wa mfuko wa Afya ya jamii (CHF) atapaswa kulipa kila mwaka mchango kiasi cha shilingi elfu kumi tu(**10,000/=)**<br>(b)Viwango hivi vinaweza kufanyiwa marekebisho na Halmashauri Wakati wowote iwapo itaonekana kuna umuhimu wa kufanya marekebisho hayo. |

**Muda wa Uanachama** . 22 (a) Mtu yeyote atabaki kuwa mwanachama wa mfuko wa afya ya jamii kila atakapolipa ada yake ya mwaka ya uanachama,na

(b) Kila mwaka unapoisha uanachama wa mtu utafikia mwisho hadi pale atakapotimiza masharti ya kifungu (a) hapo juu.

**Malipo ya papo kwa papo** . 23 (1)Mtu yeyote ambaye hatakuwa Mwanachama wa Mfuko huu atalipa malipo Ya papo kwa papo kila atakapo enda kupata matibabu katika kituo cha kutolea Huduma za Afya.

(2) Malipo ya papo kwa papo yatalipwa kwa ajili ya huduma za kiafya kama Ifuatavyo;-

a) **Shilingi elfu kumi tu (10,000/=)** katika Huduma za Afya zinazotolewa na Zahanati katika eneo lolote la Halmashauri ya Wilaya,na
b) Kwahuduma za afya zinazotolewa na kituo cha Afya na za Hosipitali iliyopo ndani ya Halmashauri ya Wilaya gharama zitatolewa kulingana na huduma inayotozwa na vituo hivyo.

**Uratibu wa Misamaha** . (24) Misamaha kwa wasioweza kulipia gharama za matibabu utatolewa na kulipiwa na Halmashauri baada ya kuzingatia utaratibu ufuatao:-

(a) Serikali ya kijiji katika vikao vyake itawatambua,kuwajadili na kupeleka kwa kamati ya Maendeleo ya kata mapendekezo ya orodha ya majina ya watu wanaostahili kupewa msamaha,ikiwa ni pamoja na kutoa mapendekezo ya vyanzo ya vyanzo vya mapato kwa ajili ya kuwalipia;
(b) Kamati ya maendeleo ya kata itawajadili wale wasiweza kulipia gharama na kuthibitisha orodha yao na kuiwasilisha kwa bodi ikiwa ni pamoja na kutoa mapendekezo ya vyanzo vya mapato kwa ajili ya kuwalipia.
(c) Bodi ya afya itapokea na kujadili mapendekezo husika na kuyawasilisha pamoja na gharama zake kwa Halmashauri kwa ajili ya kulipiwa.

**Utoaji wa Kadi kwa mwanachama** . (25)

(1) Kila mwanachama wa Mfuko atapewa kadi baada ya kulipa mchango wake wa mwaka wa **Shilingi elfu kumi tu (10000/=)**

(2) Kwa kuzingatia Sheria ya Mfuko wa afya ya jamii Sura ya 409 kila mtu atakayesamehewa kulipa mchango atapewa kadi ya Uanachamana Halmashauri italipa gharama ya kadi hiyo.

**Makosa na Adhabu** (26) Mtu yeyote ambaye:-

a) Atakwenda kinyume na masharti ya Sheria ndogo hizi;

b) Atafanya kitendo chochote ambacho kitazuia Bodi

kufanya kazi zake kwa ufanisi;

c) Atatumia vibaya mali na rasilimali za Mfuko

d) Atashindwa kwa uzembe kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa sharia ndogo hizi;

e) Atazuia utekelezaji wa sheria ndogo hizi; na atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyo zidi shilingi elfu hamsini(Tshs.50,000/=)au kuhukumiwa kifungo cha miezi kumi na miwili (12)au vyote kwa pamoja faini na kifungo.

Nembo ya Halmashauri ya wilaya imebandikwa kwenye sheria ndogo hizi kwa kuzingatia Azimio lililopitishwa kwenye mkutano wa Halmashauri.